Jina la mtahiniwa.....

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA
MTIHANI WA NUSU MUHULA KIDATO CHA KWANZA SEPTEMBA 2019

KISWAHILI

MAELEKEZO: **Muda: Saa 2 $\frac{1}{2}$**

- Mtihani huu una sehemu A, B, C na D
- Jibu maswali yote
- Zingatia maelekezo ya kila sehemu na kila swali
- Simu za viganjani haziruhusiwi

SEHEMU A (Alama 15)
UFAHAMU

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata

Mtu asiyefahamu hifadhi ya Ngorongoro atashangaa kusikia kuwa wafugaji na mifugo yao wanaishi katika hifadhi hii. Lakini kuna tofauti kati ya hifadhi ya Ngorongoro na hifadhi za Taifa kama vile Serengeti, Mikumi, Ruaha na nyinginezo.

Binadamu wanaoruhusiwa kuingia na kuishi katika hifadhi za Taifa ni walinzi wa wanyama pori, wafanyakazi wa hoteli za kitalii pamoja na watalii. Hifadhi ya Ngorongoro ni tofauti. Sio wafugaji tu wanaoruhusiwa bali kwa miaka nenda rudi wamekuwa wakiishi na kuendesha shughuli zao za ufugaji ndani ya hifadhi, wakichangamana na wanyama pori pamoja na watalii yaani matumizi mseto ya maliasili na ardhi.

Wakati mwingine magari zaidi ya 400 huingia kwenye hifadhi hii kwa siku. Hapo hapo kuna familia nyingine tu za wamasai ndani ya Ngorongoro, hifadhi ambayo miongoni mwa vivutio vyake vikuu ni kreta iliyoko ndani ya hifadhi.

MASWALI

(i) Hifadhi ya Ngorongoro ina tofauti gani ha hifadhi nyinginezo?
.....
.....

(ii) Kwa nini wamasai na mifugo yao wanaishi ndani ya hifadhi?
.....
.....

(iii) Watu gani wanapaswa kuwa katika mbuga za wanyama? (taja watu wanne)
.....
.....

(iv) Kama kila gari linaweza kubeba watu 12 ni watu wangapi wanaotarajiwa kuingia kwenye hifadhi ya Ngorongoro kwa siku?
.....
.....

(v) Nini vivutio vya watalii katika hifadhi ya Ngorongoro?(taja vivutio viwili)
.....
.....

2. Fupisha habari hii kwa maneno yasiyozidi hamsini (50)
.....
.....
.....
.....
.....
.....

SEHEMU B (ALAMA 25)
MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu mwaswali yote

3. (a) Fafanua maana ya dhana zifuatazo

(i) Silabi .....
.....

(ii) Sarufi .....
.....

(iii) Kivumishi .....
.....

(iv) Mawasiliano .....
.....

(v) Lugha .....
.....

(b) Taja maneno ya msingi matano (05) yanayopatikana katika maana ya lugha

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

(v).....

Jina la mtahiniwa.....

4. Sentensi zifuatazo zina makosa. Ziandike kwa usahihi

(i) Nilimkuta hayupo

.....

.....

(ii) Mamba kinaogelea

.....

.....

(iii) Vibaya anacheza John

.....

.....

(iv) Tafadhali nikope shilingi elfu kumi nitarudisha kesho

.....

.....

(v) Mzee Juma anapangisha kwetu

.....

.....

5. Andika kweli au si kweli katika tungo zifuatazo

(i) Lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumia ishara na hutumiwa na viumbe wote katika kuwasiliana .....

(ii) Sarufi na fasihi ni Nyanja kuu za lugha .....

(iii) Maneno yaliyoingizwa katika kamusi na kuandikwa kwa wino mzito na kupewa ufafanuzi huitwa kitomeo .....

(iv) Neno “nge” lina silabi tatu .....

(v) Irabu zote hutamkwa bila ya kizuizi cha hewa .....

(vi)

SEHEMU C (ALAMA 25)

SARUFI

Jibu maswali yote katika sehemu hii

6. (a) Tunga sentensi yenye vipashio vifuatavyo

(i) W + Ts + T + E .....

.....

(ii) N + V_1 + V_2 + T + E_1 + E_2 .....

.....

(iii) N_1 + V_1 + T + N_2 + V_2 + E .....

.....

(iv) W + t + N .....

.....

(v) N_1 + Ts + T + N_2 .....

.....

(b) Kitenzi shirikishi ni maneno yanayoonesha tabia au hali iliyokuwepo au isiyokuwepo kwa kitu au mtu fulani. Tunga sentensi tano (05) kwa kutumia vitenzi vishirikishi tofauti tofauti na pigia mstari vitenzi hivyo.

(i) .....
(ii) .....
(iii) .....
(iv) .....
(v) .....

7. (a) Jaza nafasi zilizoachwa wazi
(i) ..... ni taaluma inayoshughulikia maumbo au mjengo wa maneno katika tungo
(ii) Maneno yanayoingizwa katika kamusi na kuandikwa kwa wino mzito huitwa .....
(iii) ..... huonesha alama na vifupisho mbalimbali vinavyotumiwa katika lugha husika
(iv) Maneno yanayotaja vitu vinavyoeleweka katika fikra tu na ambavyo havishikiki wala kuonekana hujulikana kama .....
(v) ..... hutamkwa kwa kuzuia mkondo wa hewa

(b) kwa kawaida kamusi huwa na taarifa mbalimbali kwa lengo la kumsaidia mtumiaji wa lugha husika. Taja taarifa tano (05) zinazohusu neno zinazoingizwa katika kamusi
(i) .....
(ii) .....
(iii) .....
(iv) .....
(v) .....

SEHEMU D (ALAMA 35)

FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali yote

8. (a) Kutoka katika kisanduku cha majibu chagua jibu sahihi na kuliandika mbele ya namba ya maelezo yanayoelezea dhana hiyo.

Nahau, Tafsida, hadhira, vitendawili, vichekesho, fasihi andishi, tarihi au visakale, majibizano, ngonjera, ususi, fasihi, majigambo, fanani, visasili, sanaa, fasihi simulizi, methali

(i) Hupunguza ukali wa maneno au matusi katika usemi .....

(ii) Ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo katika kuumbwa, kuwasilishwa na kusambazwa kwake kwa wasikilizaji .....

(iii) Majibizano, mjadala au malumbano ya watu wawili au zaidi katika mtindo wa kishairi .....

(iv) Hadithi zinazoelezea vyanzo au chimbuko la maumbile ya binadamu, wanyama, miti au vitu visivyo na uhai .....

(v) ..... ni mtambaji wa kazi za fasihi simulizi ambaye hutumia mbinu mbalimbali kuijenga kazi yake ili kuvuta umakini wa hadhira yake

(vi) ..... Hufundisha na kuchekesha

(vii) Misemo yenye kueleza wazo lililofichika maelezo yake huwa na ukinzani wa pande mbili .....

(viii) Ufundi wa kuwasilisha mawazo yaliyo katika fikra za binadamu .....

(ix) Hurithisha na kuhifadhi amali za jamii .....

(x) Ni maigizo yenye kujitapa kwa mtu aliyefanya mambo ya kishujaa au maana .....

(b) Fasihi simulizi ina sifa mbalimbali zinazoipambanua. Taja sifa tano za fasihi simulizi

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

(v) .....

(c) Nyimbo ni kipera kimojawapo cha ushairi wa fasihi simulizi. Taja tanzu tano (05) za nyimbo

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

(v) .....

(d) Andika methali zenye maana sawa na hizi zifuatazo

(i) Ukiona zinduna ambari iko nyuma

.....

(ii) Adhabu ya kaburi aijuaye maiti

.....

(iii) Usiache mbachao kwa msala upitao

.....

(iv) Mchelea mwana kulia hulia yeye

.....

(v) Udongo uwahi ungali maji

.....

Jina la mtahiniwa……

(e) Toa maana ya nahau zifuatazo

(i) Shikilia mkia ……

(ii) Ana mkono wa birikia ……

(iii) Kuwa na mkono ……

(iv) Zunguka mbuyu ……

(v) Piga maji ……